

## Maswali

1. Nini ilikuwa ifanyike kwa Eliya?
2. Elisha alijisikia namna gani?
3. Mbona Elisha hakumuacha Eliya?
4. Manabii wengine walijuaje atakachofanya Mungu?
5. Mbona Elisha aliwauliza wasilizungumzie?
6. Eliya alifanya nini kwa mto Yordani?
7. Elisha aliuliza apewe nini?
8. Mbona ilikuwa vigumu kwa Eliya kumpa?
9. Tunajuaje alipata mgawo wa roho maradufu?
10. Watu wanajuaje sisi ni watu wa utawa?

## Majibu

1. Eliya alikuwa achukuliwe na Mungu ili aende apumzike kabla ya kufa.
2. Elisha alihuzunika sana kwa sababu hakutaka kumuacha rafiki wa utawa.
3. Elisha hangemwacha Eliya kwa sababu aliogopa kwamba Eliya atachukuliwa kama hayupo.
4. Manabii walijua kitakachofanyika kwa sababu Mungu huwapa manabii ujumbe wake.
5. Elisha hakutaka izungumziwe kwa sababu alijua Mungu akinena kitu lazima kitendeke tena alijua atakosa rafiki.
6. Eliya alipiga maji ya mto kwa vazi lake na muujiza ukafanyika, maji yakagawanyika.
7. Elisha aliuliza mgawo maradufu wa roho ya Eliya.
8. Eliya hangeweza kumpa kwa sababu nguvu zote zatoka kwa Mungu sio kwa Eliya.
9. Tunajua alipata roho kwa sababu aliona Eliya akichukuliwa na angefanya miujiza kama Eliya.
10. Watu watajua tuna utawa ikiwa tutazungumza na kutenda mambo ya Mungu.

## SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 2



# 24 Elisha anachuuwa ushukani kutoka kwa Eliya

## Marejeo

2 Wafalme 2:1—15

## Kiini cha somo

Kuwa na imani hata wakati rafiki zetu wanatuacha.

## Maneno maalum

1. Eliya + nabii + pumzika + chukuliwa na Mungu + Elisha ana wasiswasi + kuwa karibu.
2. Betheli + kaa hapa + sitakuwacha + chukuliwa + usiyazungumzie.
3. Yeriko + kaa hapa + sitakuwacha + Eliya achukuliwa + usiyazungumzie.
4. Mto Yordani + vazi + piga + maji yanagawanyika.
5. Nikufanyie nini + roho mara dufu + kigumu + ukiniona.
6. Gari na farasi za moto + kisulisuli + anga + huzunika.
7. Nabii 50 + chagua + vazi + omba + piga + maji yatawanyika + Mungu alikuwa naye.

**24.1** Mda wa Eliya kama nabii wa Mungu ulikuwa unayoyoma. Alikuwa amefanyia Mungu kazi ya kweli na ilipaza apumzike. Elisha aliyetakiwa kuchukuwa ushukani alijua siku yake inakuja. Hivi karibuni bwana wake atachukuliwa na yeye ndie atakuwa nabii wa Mungu. Elisha aliogopa kwa sababu ilikuwa kazi ngumu na hakujiamini kama atafanya. Alikaa karibu na Eliya ili Eliya asichukuliwe kama hayuko tayari kwa hiyo kazi.

**24.2** Siku moja Eliya akamwambia, “Mungu ameniambia niende kwa mji wa Betheli- wewe kaa hapa mimi niende.” Elisha alimjibu, “Hapana sitakuacha!” Manabii wa shule ya Betheli walimuuliza kama alijua kwamba Eliya atachukuliwa na Mungu. Alijibu, “Ndiyo lakini msilizungumzie hili jambo.” Elisha alikuwa na huzuni, hakutaka wawachane na rafiki wake wa karibu. Eliya alikuwa amemsaidia Elisha kuwa karibu na Mungu na alitaka waendeleo kuwa marafiki.

**24.3** Eliya akamwambia, “Mungu ameniambia niende Yeriko, wewe kaa hapa mini niende.” Elisha alimjibu, “Hapana, sitakuacha!” Walipofika Yeriko manabii was shule ya Yeriko walimuuliza kama alijua kwamba Eliya atachukuliwa na Mungu. Alijibu, “Ndiyo lakini msilizungumzie hili jambo.”

**24.4** Tena Eliya akamwambia, “Mungu ameniambia niende kwa mto Yordani, wewe kaa hapa.” “Hapana!” Elisha alisema, “Sitakuacha!” wakaenda wote. Walipofika mto wa Yordani walitaka kuvuka. Eliya akachukuwa vazi lake na kuipigia maji. Papo hapo maji yaligawanyika na wakavuka mto mkavu.

**24.5** Eliya akamuuliza Elisha, “Nikufanyie nini kwa sababu punde tu nitachukuliwa na Mungu?”

Elisha aliuliza apewe roho wa Eliya maradufu ili awe mtu wa Mungu kama Eliya. Eliya alimjibu kwamba ilikuwa jambo ngumu kwa sababu nguvu zote zinatoka kwa Mungu, sio yeye. Eliya akamwambia, “Ikiwa utaniona nikichukuliwa, utapata la sivyo hautapata.”

**24.6** Walipokuwa wakitembea gari la moto lililokuwa likifutwa na farasi wa moto, liliwaganyisha Eliya na Elisha. Eliya alichukuliwa akaenda juu kwa kisulisuli. Elisha alihuzunika sana, akalia kwa sauti na kurarua nguo zake.



**24.7** Manabii 50 walioyaona haya yote walimuangalia Elisha ili wajue kama kweli amepewa kazi ya Eliya. Elisha alichukuwa vazi la Eliya na kuenda kwa mto Yordani. Alikuwa bado na huzuni kwa kumpotoza rafiki wa utawa aliyekuwa akimsaidia. Lakini aliamua kujaribu, kwa hivyo akaomba Mungu na kupiga maji na hilo vazi la Eliya, maji yaligawanyika. Hapo Elisha alijua kwamba Mungu ako nae na atamsaidia kwa kazi hii mpya. Manabii 50 pia wakaona kwamba Mungu alikuwa na Elisha. Walimkimbilia kumlaki na kuwa rafiki wake.

## **OMBI**

Ee Mungu tusaidie tuwe na nguvu wakati mtu tunayempenda, tunayemheshimu na kumfuata akichuliwa kutoka kwetu. Tusaidie tuwe kama hao jinsi walivyo onyesha upendo kwako. Tusaidie tujue hata kama wameenda, wewe bado uko nasi. Tukikurudia wewe, utatusaidia tuwe na utawa. Amina.